

Mtanzania Juni 30, 2011

Kunradhi Goyagoya

KATIKA gazeti la MTANZANIA la Mei 2, 2010, kulichapishwa habari iliyosomeka, "Mpambe wa mgombea abambwa kwa rushwa".

Katika moja ya aya tulimtaja Agatoni Goyagoya kwamba alikuwa pamoja na huyo mpambe aliyekamatwa, lakini yeye alifanikiwa kukimbia.

Goyagoya alilalamika katika Baraza la Habari Tanzania (MCT). Juni 16, 2011 Kamati ya Maadili ya MCT chini ya Mwenyekiti wake, Jaji Mark Bomani, ilisikiliza shauri hilo na kulitolea uamuzi.

Ilibainishwa kuwa habari hiyo ilikuwa na upungufu kadhaa, ukiwamo wa kutomhoji Goyagoya baada ya kupata taarifa hiyo.

Aidha, MTANZANIA iliamuriwa kumwomba radhi Goyagoya na kumlipa gharama za matumizi alizoingia baada ya kuandikwa kwa habari hiyo.

Tunachukua fursa hii kumwomba radhi Goyagoya kwa usumbufu uliosababishwa na habari hiyo. Tunachukua uamuzi huu baada ya kujiridhisha kuwa habari hiyo ilikuwa na upungufu wa kitaaluma. Mata-rajio yetu ni kuhakikisha kuwa makosa ya aina hiyo hayatokei tena. Kunradhi Ndugu Goyagoya na wote walicathiriwa kwa namna moja au nyingine na habari hiyo.

MHARIRI